

JINA _____

KIDATO _____

NAMBARI _____

**ALLIANCE HIGH SCHOOL
MTIHANI WA MWIGO WA KISWAHILI
KIDATO CHA NNE 2017
KARATASI YA 3 102/3
FASIHI
MUDA SAA 2½**

MAAGIZO.

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja au kitabu kimoja.
5. Kila swali lina alama 20.

SEHEMU A: SHAIRI

Swali la Lazima

SHAIRI A

Wewe,
Utazame mlolongo wa waja unaoshika njia ikiwapo;
Unaofuata pembe za bara bara zisokuwapo,
Kwenda kuisaka auni,
Kuitafuta kazi inayowala chenga.

Itazame migongo ya wachapa kazi,
Watokwao na jasho kapakapa na,
Wanaotafunwa uhai na jua liso huruma.

Wakiinua vyuma na mangunia,
Wakiinua makontena,
Wakichubuka mashambani,
Wakiumia viwandani,
Wakiteseka makazini,

Halafu
Uangalie ule ujira wa kijungu meko,
Mshahara usokifu haja,
Nguo zisizositiri miili dhaifu,
Kilo chao kisichokuwa na machozi,
Na
Ujiangalie
Mwili wako unaomereta ujana wa ufanisi,
Gari lako la kifahari lililozibwa vioo,
Jumba lako la kujishasha kama uwanja mdogo,
Malaki ya pesa unayomiliki,
Ujiitapo mwajiri kwa raha, hunusi usaha wa hali yao?

SHAIRI B

Dunia kitendawili, hakuna ateguaye;
Dunia kama tapeli, hadaa nyingi ujuye;
Dunia mwenye akili, inampiku nay eye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia na yake hali, hupumbaza hatimaye;
Dunia ina akili, huiwezi sichezeye;
Dunia uwe na mali, huiwezi dhorubaye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia wenye muali, ambao waichezeye;
Dunia kipigo kali, huwakumba hatimaye;
Dunia wakaja kuli, "menipata nini miye?"
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Maswali.

- (a) Taja nafsineni katika mashairi yote mawili. (al. 2)
- (b) Eleza sababu za utungo A kuitwa shairi. (al.4)
- (c) Linganu mashairi haya kiumbo. (al.3)
- (d) Ukitoa mifano kutoka shairi A, bainisha matumizi ya;
(i) Kweli-kinzani (al.2)
(ii) Mishata
- (e) Bainisha toni/lahani katika mashairi haya. (al.2)
- (f) Shairi B linaweza kuwa katika bahari tatu. Thibitisha. (al.3)
- (g) Toa mfano mmoja kutoka kila shairi kuonyesha idhini ya ushairi. (al.2)
- (h) Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika. (al.2)
- (i) Dunia kama tapeli.
- (iii) Kuisaka auni

SEHEMU B: RIWAYA

K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea.

Jibu swali la 2 au la 3.

1. Jadili maudhui ya Ukosevu wa utu katika riwaya ya Kidagaa kimemwozea. (al.20)
2. (a) "Afrika imevikwa maneno matupu". Eleza muktatha wa dondoo hili. (al.4)
(b) Msemaji wa maneno haya amechukua hatua kadhaa kukabiliana na tatizo la jamii yake kuvikwa maneno matupu. Jadili hatua hizo kwa kutoa mifano mwafaka. (al. 6)
(c) Imani ni kielelezo cha vijana waliowajibika. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea mifano kutoka kidagaa kimemwozea. (al.10)

SEHEMU YA C. TAMTHILIA
T. AREGE: MSTAHIKI MEYA.

Jibu swali la 4 au la 5.

3. Mwandishi wa tamthilia ya Mstahiki Meya ametumia mbinu zifuatazo za lugha kwa ufanisi mkubwa. Jadili.
- (a) Jazanda. (al.4)
 - (b) Kinaya (al. 4)
 - (c) Utatu (al.4)
 - (d) Taswira (al.4)
 - (e) Majazi (al.4)
4. Fafanua jinsi maudhui yafuatayo yalivyojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
- (a) Subira (al.4)
 - (b) Uoga (al.4)
 - (c) Dini (al.4)
 - (d) Usaliti (al. 4)
 - (e) Kiburi/majigambo. (al.4)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI.

K. Walibora na S.A. Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

Jibu swali la 5 au la 7.

5. Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ukirejelea hadithi, 'Ndoa ya Samani' na Mwana wa Darubini. (al.20)
6. Hadithi ya kobe ni muhtasari wa matukio katika hadithi ya 'KIKAZA' Thibitisha. (al.20)

SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI.

7. (a) Kwa kutumia mifano mwafaka, eleza maana ya vipera hivi katika fasihi simulizi. (al. 8)
- (i) Nahau

(ii) Misemo

(iii) Misimu

(iv) Lakabu

(b) Kipera cha methali hutumia tamathali za usemi katika uwasilishaji wake.

Taja mfano mmoja wa methali zinazotumia mbinu hizi. (al.4)

(i) Takriri

(ii) Chuku

(iv) Istiara

(v) Tashbihi

(c) Fumbua mafumbo haya: (al.2)

(i) Anijengaye hana haja nami. Aninunuaye hanitumii. Naye anayenitumia hanioni.

Jibu _____

(ii) Kulitokea kifo cha mamane samba. Simba alimfukuza ngiri katika maombolezi.

Jibu _____

(d) Jadili dhima sita (6) za vitendawili katika fasihi simulizi. (al.6)

Kifa la kheri. Idara ya Kiswahili AHS